


DIWANI YA HADITHI ZA WANYAMA

Hadithi Fupi 50 kwa Watoto

Juzuu
ya **1**



Diwani ya Hadithi za Wanyama

Juzuu ya Kwanza

Yaliyomo:

Akili ni Mali	4
Asasi Mlafi	18
Anasi Mvivu	31
Anasi Mwenye Wivu	49
Bibi, Sungura na Tembo	63
Chura na Nyoka	77
Fana Anawapenda Wanyama	95
Fisi, Sungura na Beseni	105
Hasira ya Kuku	119
Jimbi Anadanganya	133
Jinsi Chura Alivyopata Ngozi Yake	147
Kima na Fisi	161
Kima na Kiangazi Kibaya	175
Kimbia Sungura, Kimbia!	193
Kobe na Sungura	211
Kuhesabu Paka	228
Kuku na Jongoo	241
Kusema Asante!	255
Kutotii!	273
Kuwaheabu Wanyama	287
Magezi na Kasiira	297
Mamba Aliyekuwa na Njaa	319
Mamba na Mbwa	327
Mbweha Asiye na Shukrani	341
Meno Aina Gani?	358
Mfalme Mbaya	369

Yaliyomo:

Mtoto na Korongo	389
Mvulana Asiyetii	399
Mwanamume na Mwanamke wa Kwanza	413
Ng'ombe Wetu, Pendo	425
Ni Nani Atakuwa Mfalme?	439
Nyani Aliyekuwa Chifu	457
Nyumbu	471
Panya na Paka	489
Petros Ampata Rafiki	507
Punda na Fahali	521
Siafu na Njiwa Mvivu	535
Simba, Jike, na Mbuni	549
Sokwe na Mamba	567
Sungua Amdanganya Tembo	585
Sungura na Fisi	601
Sungura na Fisi Wanapanda Mimea	619
Tarik na Rafiki Yake	637
Ujanja wa Sungura	651
Ulimwengu Wetu	665
Vituko vya Ng'ombe Shujaa	679
Wanyama wa Kufungwa	691
Wanyama Wapata Miguu	699
Wapi Paka Wangu?	719
Watazame Wanyama	729



Kitabu hiki kimeandaliwa na maktaba.org, mradi wa Elimu Yetu Development Organization unaolenga kukuza utamaduni wa usomaji Afrika Mashiriki. Unaweza kupakua hadithi zote na kumsomea mtoto kila siku kabla ya kulala. Hadithi na picha zilizopo ndani zinatoka African Storybook. Tunawashukuru sana AfricanStorybook.org kwa kutoa vitabu bure kwa watoto wote wa Afrika. Ukitaja waandishi, **inaruhusiwa** kunakili, kuiga, kupiga chapa, kutafsiri na kusambaza kitabu hiki kwa njia zote, popote ulipo. Kitabu hiki na vitabu vingi zaidi vinapatikana bure kwenye tovuti yetu, maktaba.org.



Kitabu hiki kimeandaliwa na:



Elimu Yetu

Soma zaidi:




Akili ni mali


Ursula Nafula
Abraham Muzee




Kiswahili



Sokwe alimkuta
Mamba kando ya
mto mkubwa.



Mamba akasema,
"Nina maumivu.
Tafadhali nisaidie."



Sokwe akamwuliza,
"Unahitaji nini?"



Mamba akamjibu,
"Usiponipatia
moyo wako,
sitapona."




Sokwe akasema,
"Kwanza nibebe
hadi upande wa
pili wa mto."



Mamba akambeba
Sokwe mgongoni
wakavuka mto.




Sokwe akasema,
"Ninahitaji kisu ili
niukate moyo
wangu."



Wakati huo huo,
upepo mkali
ukaanza kuvuma.




Mamba akainuliwa
juu karibu
amuangushe
Sokwe.



Sokwe alipoiona
nchi kavu,
akamwambia
Mamba
aharakishe.



Ghafla, Sokwe
akaurukia mti.



Mamba
akakasirika
akasema,
"Ulinidanganya!
Utajuta!"

Akili ni mali

Author - Ursula Nafula

Illustration - Abraham Muzee

Language - Kiswahili

Level - First words

© African Storybook Initiative 2017

Creative Commons: Attribution 4.0

Source www.africanstorybook.org

Anansi mlafi

Ursula Nafula

Wiehan de Jager




Kiswahili



Anansi aliwakuta
kunguru wakila
makuyu.

Yeye pia alitaka
makuyu.



Kunguru
walimpatia Anansi
makuyu.




Kunguru
walimwambia,
"Sasa njoo uchume
makuyu nasi."



Walienda kuchuma
makuyu pamoja.

Lakini Anansi
alichukua makuyu
yote.



Anansi aliruka.

Alianguka ndani ya
mto uliojaa
mamba.



Anansi alisema,
"Mimi ni mmoja wa
jamaa zenu."

Hakuliwa.




Anansi alijifanya
kuwa anakunywa
maji chafu kama
mamba.




Mamba
walimwamini
Anansi.

Walimualika kukaa
nao.



Anansi alisema,
"Nitakaa, lakini,
hebu kwanza
niilete famalia
yangu."



Mamba alimbeba
Anansi hadi ukingo
wa mto.



Anansi alitoroka.

Mamba bado
anamsubiri hadi
leo.

Anansi mlafi

Author - Ghanaian folktale

Translation - Ursula Nafula

Illustration - Wiehan de Jager

Language - Kiswahili

Level - First words

© African Storybook Initiative 2014

Creative Commons: Attribution 4.0

Source www.africanstorybook.org

ASb
approved

Anansi mvivu

Brigid Simiyu
Wiehan de Jager

Kiswahili

Anansi ni buibui mvivu.



Anapenda chakula,
lakini hapiki kwani
ni mvivu.

Anansi anamtembelea Sungura.

Anaomba wale mboga pamoja.



"Nisaidie
kukoroga,"
Sungura anasema.

Anansi hataki, ni
mvivu.

"Nitarudi baadaye," Anansi anasema.



Anafunga utando
mguuni na kwenye
chungu cha
Sungura.

"Vuta utando mboga zitakapoiva," Anansi anasema.



"Kima, naomba
nile maharage
nanyi?"

"Tusaidie kufanya
kazi."

"Nitarudi," Anansi anasema.

Anafunga utando zaidi.




"Ngiri, tule viazi
pamoja?"

"Nisaidie
kuvitayarisha,"
Ngiri anamjibu.

"Nitarudi," Anansi anasema.


Anafunga utando zaidi.



Hatimaye, kila
mguu wa Anansi
umefungwa
kwenye chungu.

Anansi anavutwa kwenye mguu wa 2.

Halafu mguu wa 3.



Miguu yote 8
inavutwa!

"Acheni kuvuta!"
Anansi analia.

Hakuna anayemsikia Anansi.

Utando unakatika mmoja mmoja.



Ndiyo sababu
buihui wote wana
miguu mirefu
myembamba.

Anansi mvivu

Author - Ghanaian folktale

Translation - Brigid Simiyu

Illustration - Wiehan de Jager

Language - Kiswahili

Level - First words

© African Storybook Initiative 2014

Creative Commons: Attribution 4.0

Source www.africanstorybook.org



Anansi mwenye wivu

Ursula Nafula

Wiehan de Jager



Anansi na Sungura
walikuwa marafiki.

Anansi alionea
wivu mali ya
Sungura.



Anansi alimfukuza
Sungura.

Akachukuwa
shamba lake.



Anansi aliuza
mazao yote.

Alipata pesa nyingi.



Anansi alirudi
nyumbani.

Alikibeba kikapu
kichwani.



Anansi alikiweka
kikapu chini.

Alienda kujikinga
asinyeshewe.



Muvua ilisababisha
mafuriko.

Anansi alijificha
shimoni.



Tai alikiona kikapu.

Alikifunika kwa
mabawa yake.



"Kikapu hiki ni changu," Tai alisema.

"Ni changu!"
Anansi alipiga kelele.



Tai alisema,
"Nilipata mahindi
na pesa bila
mwenyewe."



Chifu na wazee
wake walichukuwa
muda kuamua
nani alisema
ukweli.



Hatimaye,
walisema, "Tai
anasema ukweli.
Kikapu ni chake."



Sungura alirudi
katika shamba
lake.

Anansi hakuwa na
pesa wala marafiki.

Anansi mwenye wivu

Author - Ghanaian folktale

Translation - Ursula Nafula

Illustration - Wiehan de Jager

Language - Kiswahili

Level - First words

© African Storybook Initiative 2014


Creative Commons: Attribution 4.0

Source www.africanstorybook.org



Bibi, Sungura na Tembo


Brigid Simiyu
Marleen Visser



Bibi alianza,
“Sungura na
Tembo walikuwa
marafiki tena
majirani.”



Sungura alipenda
uyoga lakini
alikuwa mvivu
sana. Hakulima.



Sungura hakupata
uyoga.

Alianza kuiba ndizi
za Tembo.



Tembo aliimba,
“Nitamshika
mwizi!”

Sungura aliogopa.



Kima alimchungia
Tembo shamba
lake.

Lakini, Sungura
hakuiba.



Tembo alienda
kutazama.

Sungura alijificha
ndani ya matawi
ya maboga.



Tembo aliangalia
kila mahali.


Hakumpata mwizi.



Siku nyingine,
Sungura alijificha
ndani ya boga
kubwa.



Tembo aliliona hilo
boga kubwa
akalimeza.



Boga lilisonga
tumboni mwa
Tembo.



Tembo alitema
boga.

Sungura alitoka
ndani akatoroka.



Bibi alisema, “Na huo ndio mwisho wa hadithi.”

Bibi, Sungura na Tembo

Author - Mutai Chepkoech

Translation - Brigid Simiyu

Illustration - Marleen Visser

Language - Kiswahili

Level - First words

© African Storybook Initiative 2016

Creative Commons: Attribution 4.0

Source www.africanstorybook.org



Chura na Nyoka

Brigid Simiyu
Rob Owen

Kiswahili



Chura na Nyoka
walikuwa marafiki.



"Njoo twende
tukamtembelee
mamangu." Chura
alimwalika Nyoka.



"Asante, lakini nani
atatuchungia
makao yetu?"
Nyoka alimwuliza
Chura.



"Nitawachungia
makao yenu," Kima
alijitolea.



Chura aliweka
mchwa mkobani
kumpelekea
mamake.



Chura na Nyoka
waliondoka
asubuhi wakaingia
msituni.



Waliwakuta
vichakuro. Nyoka
aliwaogopa.



Chura alimlinda
rafiki yake Nyoka.



Walipofika kwa
mamake Chura,
walikuwa wakihisi
njaa sana.



Walinawa
wakajitayarisha
kwa chakula.



"Nyoka, tafadhali
keti wima." Chura
alimwambia
rafikiye.



Nyoka alijaribu kuketi wima, lakini hakuweza. Yeye si kama chura.



"Siwezi kuketi wima
kama chura,"
Nyoka alimjibu.



Chura hakumsikiza
Nyoka. Alianza
kukasirika.



Nyoka pia
alikasirika
akasema,
"Hunielewi. Heri
nirudi nyumbani."



Nyoka aliondoka
kwa hasira.
"Nilidhani Chura ni
rafiki yangu."
Aliwaza.

Chura na Nyoka

Author - John Emongot

Translation - Brigid Simiyu

Illustration - Rob Owen

Language - Kiswahili

Level - First words

© African Storybook Initiative 2016


Creative Commons: Attribution 4.0

Source www.africanstorybook.org

Fana anawapenda wanyama

Ursula Nafula
Jesse Breytenbach






Fana na familia
yake wanaishi
mjini.



Fana ana paka,
kuku wawili, mbuzi
na njiwa.



Siku moja Fana aliwaona watoto wakiwarushia njiwa mawe.



Fana alikimbia
akisema, "Acheni
kutupa mawe."



Fana aliwachukua
wale njiwa
akawapeleka
nyumbani.



Aliwalisha.

Aliwaambia wazazi
vile alivyowaokoa.



Fana na wazazi
wake waliwapeleka
njiwa kutibiwa.



Fana huwaambia
wenzake,
"Wanyama ni
marafiki zetu.
Tunawalinda."

Fana anawapenda wanyama

Author - Foziya Mohammed

Translation - Ursula Nafula

Illustration - Jesse Breytenbach

Language - Kiswahili

Level - First words

© African Storybook Initiative 2017

Creative Commons: Attribution 4.0

Source www.africanstorybook.org


Fisi, Sungura na Beseni

Brigid Simiyu
Salim Kasamba




Kiswahili

Fisi na Sungura walikuwa marafiki.



Sungura alikuwa
na punda wake.

Alikuwa pia na
beseni ndogo
nyekundu.



Sungura
alimwomba Fisi
beseni yake kubwa
ya bluu.



Fisi alihitaji beseni
yake ili afue nguo
zake.


Fisi alisema, “Ninahitaji beseni yangu kubwa.”



“Beseni yako ilizaa mtoto.” Fisi alibeba beseni mbili.




Siku nyingine,
Sungura aliomba
tena beseni ya Fisi.



Fisi alipoendea
beseni yake,
alipata ujumbe
mbaya.

"Beseni yako ilifariki." Fisi hakuweza kuamini hili.



Fisi aliwaita
wanyama
wakubwa waamue
ukweli.



"Viumbe vilivyo hai
na vinavyozaa, pia
hufa," Sungura
alisema.

Wanyama walikubali. Fisi aliipoteza beseni yake.

Fisi, Sungura na Beseni

Author - Charles Katiwa Kiema

Translation - Brigid Simiyu

Illustration - Salim Kasamba

Language - Kiswahili

Level - First words

© African Storybook Initiative 2016

Creative Commons: Attribution 4.0


Source www.africanstorybook.org

Hasira ya Kuku

Ursula Nafula
Magriet Brink



Kiswahili



Kuku na Jongoo
walikuwa marafiki.

Walitembea
pamoja kila
mahali.



Siku moja,
walienda kucheza
mpira wa miguu.



Kuku alisema,
"Nitakuwa
golikipa."

Jongoo alianza
kucheza mpira.




Jongoo alicheza
mpira kwa ustadi.

Alifunga bao la
kwanza.



Kuku alishangaa
akasema,
"Haiwezekani!"

Alikasirika sana.



Kuku alifikiria
namna ya
kumwadhibu
Jongoo.

Aliamua kummeza.



Kuku alikutana na
Mamake Jongoo.

"Wapi
mwanangu?"
Mamake Jongoo
aliuliza.



Jongoo aliyemezwa
alilia, "Mama
nisaidie. Kuku
amenimeza."



Kuku
hakupendezwa na
ladha ya Jongoo.

Alihisi
kichefuchefu.



Kuku aliwaza,
"Nitafanyaje?"

Aliamua kukohoa
ili amteme Jongoo.



Jongoo
alipotemwa,
alitafula njia ya
kutoroka.

Hakuamini
alichotendewa.



Tangu siku hiyo,
urafiki kati ya kuku
na jongoo uliisha.

Hasira ya Kuku

Author - Winny Asara

Translation - Ursula Nafula

Illustration - Magriet Brink

Language - Kiswahili

Level - First words

© African Storybook Initiative 2014

Creative Commons: Attribution 4.0

Source www.africanstorybook.org



Jimbi adanganya Ursula Nafula Wiehan de Jager




Zamani, wanyama
waliishi pamoja.

Walikutana
kumchagua
mfalme.



Jimbi alitaka kuwa mfalme.

Alidanganya kuwa alikuwa na moto kichwani.




Wanyama wengine
walimwamini Jimbi.

Walimchagua
kuwa mfalme.



Msimu wa mvua
ulifika.

Kila kitu kilikuwa
maji na baridi.



Sungura aliuliza,
"Tutaupata moto
wapi tujipashe
joto?"



Kima alisema,
"Tutaupata kwenye
kichwa cha Jimbi."



Wanyama
walimtuma Mbwa
Mwitu kuleta moto
kutoka kwa
mfalme wao.



Mbwa Mwituu
alienda kuuchukua
moto bila
kumuamsha Jimbi.



Mbwa Mwitu
aliweka nyasi kavu
kichwani.


Hazikushika moto.



"Mwamshe mfalme Jimbi! Tunahitaji moto sasa," Mbwa Mwitu alisema.



Jimbi hakuwa na
moto wa kumpatia
Mbwa Mwitu.



Kutoka siku hiyo,
mbwa mwitu hula
jimbi.

Jimbi adanganya

Author - Vincent Afeku

Translation - Ursula Nafula

Illustration - Wiehan de Jager

Language - Kiswahili

Level - First words

© African Storybook Initiative 2015

Creative Commons: Attribution 4.0

Source www.africanstorybook.org



Jinsi chura
alivyopata
ngozi yake
Brigid Simiyu
Rob Owen



Mod alikuwa
amechoka kuishi
majini.



"Jihadhari. Ngozi
yako itanyauka,"
Kasa alimwonya.



Lakini, Mod alitaka
kujua.

Aliruka akaenda
zake.



Alitazama kila
mahali.



Alikuta kinyonga
wa kizambarau.

Alikuwa kando ya
dimbwi la maji.



Kinyonga aligeuka
rangi ya waridi!

Mod aliruka mbali
naye.



Alimwona fisi
akikoka moto.



Moto ulienea
karibu na Mod.

Aliogopa.



Moto uliichoma
ngozi yake.

Aliruka ndani ya
dimbwi la maji.



Lakini ngozi yake
ilikuwa tayari na
malengelage.



Mod alipata ngozi
kavu na mbaya.

Alianza kuishi
miambani.



Vyura wachache
wana ngozi
nyororo.

Wanaishi majini.

Jinsi chura alivyopata ngozi yake

Author - Alice Mulwa

Translation - Brigid Simiyu

Illustration - Rob Owen

Language - Kiswahili

Level - First words

© African Storybook Initiative 2015


Creative Commons: Attribution 4.0

Source www.africanstorybook.org



Kima na Fisi

Ursula Nafula
Salim Kasamba



Kima na Fisi
waligombana.

Walitaka ushauri
wa Hakimu.



Hakimu aliwaza,
"Kima atakula
mahindi yangu. Fisi
atakula mifugo
wangu!"



Mwishowe, Hakimu
aliwaambia,
"Tafuteni ushauri
wa wazee wa kijiji."



Wazee pia
waliogopa.

Hawakuamua kesi
kati ya Kima na
Fisi.



Wazee
waliwaambia Kima
na Fisi, "Kesi hii ni
ngumu sana."




Wazee walisema,
"Tafuteni ushauri
kutoka kwa
mwanamke
maskini."



Mwanamke
maskini alikubali
kuamua kesi yao.

"Sina mali ya
kupoteza."



Alimwambia Fisi,
"Wewe
unaheshimiwa, ni
mkubwa na ni
shujaa. Acha
ugomvi."



Fisi alijibu,
"Umesema ukweli.
Nitakomesha huu
ugomvi. Sitaki
aibu."



Mwanamke
alimwambia Kima,
"Wewe ni mwerevu.
Acha ugomvi."

Kima alikubali.



Aliwaambia,
"Mmekubali
kukomesha
ugomvi. Ni vyema
kusameheana."



Mwanamke
maskini
alisuluhisha tatizo
lao.

Kima na Fisi

Author - Mulualet Daba

Translation - Ursula Nafula

Illustration - Salim Kasamba

Language - Kiswahili

Level - First words

© African Storybook Initiative 2017

Creative Commons: Attribution 4.0


Source www.africanstorybook.org

Kima na kiangazi kibaya

Brigid Simiyu




Kiswahili




Mvua haikunyesha.
Ardhi ilikuwa kavu
sana.




Kima aliondoka
nyumbani kutafuta
maji na chakula.




Alipitia milima na
mabonde.



Alifika sehemu
iliyoitwa Tirkol.




Kima alifurahia
mahali hapa sana.




Alikula matunda
akanona. Lakini,
aliwakosa
wenzake.




Kwa hivyo Kima
alifunga safari
kurudi nyumbani.




Kima wengine
walifurahi
kumwona.



Walimuuliza, "Hii ni
sehemu gani iliyo
na matunda?"



“Nitawapeleka
huko,” Kima
aliwajibu.




Kima wote
walipenda Tirkol.
Waliamua kuishi
huko milele.




Lakini kima wa
Tirkol walikuwa na
wasiwasi.




“Kima wageni
watakula matunda
yetu yote,”
walisema.



Kima wa Tirkol
walienda
kuwavamia kima
wageni.



Kima mzee aliuliza,
“Mbona vita?
Matunda
yatatutosha!”



Ilikuwa ukweli.
Kima waliamua
kuishi pamoja kwa
amani.

Kima na kiangazi kibaya

Author - Alice Edui

Translation - Brigid Simiyu

Illustration -

Language - Kiswahili

Level - First words

© African Storybook Initiative 2016

Creative Commons: Attribution 4.0

Source www.africanstorybook.org



Kimbia
Sungura,
Kimbia!
Brigid Simiyu
Wiehan de Jager




Sungura alikuwa
amelala chini ya
mti.

Tofaa likaanguka
kutoka mti ule.



Sungura akasikia
sauti ikisema,
"Kimbia Sungura,
kimbia!"



Sungura akasema,
"Kitu kilianguka
nikasikia, 'Kimbia
Sungura kimbia!'"



Kuku alianza
kukimbia aliposikia
alivyosema
Sungura.



Wakamwambia
Mbwa, "Sungura
alisikia kitu
kikianguka naye
akakimbia."



Mbwa akaanza
kukimbia pamoja
na Sungura na
Kuku.



Mbwa
akamwambia
Farasi, "Sungura
alisikia kitu
kikianguka naye
akakimbia."



Farasi akaanza
kukimbia pamoja
nao.



Punda akawauliza,
"Mbona
mnakimbia?"

Farasi akamjibu,
"Sijui."



Punda pia akaanza
kukimbia pamoja
nao.



Punda
akamwambia
Ng'ombe, "Sungura
alisikia kitu
kikianguka
akakimbia."



Ng'ombe alikuwa
na wasiwasi.

Akaanza pia
kukimbia pamoja
nao.



Ng'ombe
akamwambia
Paka, "Sungura
alisikia kitu
kikianguka naye
akakimbia."



Paka akaanza
kukimbia na
wanyama wengine.



Walimkuta
mvulana
akawauliza, "Kwani
hamjui
kilichotendeka?"



"Ni mimi
niliyesema, "Kimbia
Sungura kimbia!"

Mvulana alicheka.

Kimbia Sungura, Kimbia!

Author - Phumy Zikode

Translation - Brigid Simiyu

Illustration - Wiehan de Jager

Language - Kiswahili

Level - First words

© African Storybook Initiative 2015


Creative Commons: Attribution 4.0

Source www.africanstorybook.org



Kobe na
Sungura
Ursula Nafula
Padmanabha

Kiswahili



Hapo zamani,
Sungura na Kobe
walishindana mbio.




Wanyama wengine
walitazama
mashindano hayo.



Sungura
alimshinda Kobe.


Hata hivyo,
hakujivuna kwa
kuwa mshindi.



Kobe na Sungura
waliendelea kuwa
marafiki.



Mfalme Simba
aliwatuma Kobe na
Sungrua kwa
mfalme jirani.



Kobe na Sungura
waliondoka
kutimiza
walivyotumwa.



Mfalme Simba
aliwasubiri Kobe
na Sungura kurudi.




Barabara
waliyotumia ilijaa
mawe na miiba.




Kobe na Sungura
walitembea,
wakatembea.

Walipumzika na
kuzungumza.



Walijadili jinsi ya
kusaidiana.



Sungura alimbeba
Kobe walipopita
kwenye
miiba.



Walipofika mtoni,
Kobe alimbeba
Sungura
wakavuka.




Kobe alitembea
haraka sana.

Sungura alijishikilia
mgongoni.



Kobe na Sungura
walijadiliana na
mflame jirani.



Walirudi nyumbani
haraka sana.

Kobe na Sungura
walikuwa marifiki
wakubwa!

Kobe na Sungura

Author - Venkatramana Gowda and Divaspathy Hegde

Translation - Ursula Nafula

Illustration - Padmanabha

Language - Kiswahili

Level - First words

© Pratham Books 2014

Creative Commons: Attribution 4.0

Source www.africanstorybook.org

Original source www.prathambooks.org



Kuhesabu paka

African Storybook

Jesse Breytenbach



Kiswahili



Paka wangapi?

Paka sufuri 0.




Paka wangapi?

Paka mmoja 1.



Paka wangapi?

Paka wawili 2.



Paka wangapi?

Paka watatu 3.



Paka wangapi?

Paka wanne 4.




Paka wangapi?

Paka watano 5.



Paka wangapi?

Paka sita 6.




Paka wangapi?

Paka saba 7.



Paka wangapi?

Paka wanane 8.



Ni nini hiki
tunachoona?

Mtoto wa paka
amekwama mtini!

"Nitamuokoa!"



"Mama, tunaweza
kumfuga paka
mmoja zaidi!"

Paka wangapi?

Paka tisa 9.

Kuhesabu paka

Author - Nina Orange

Translation - African Storybook

Illustration - Jesse Breytenbach

Language - Kiswahili

Level - First words

© African Storybook Initiative 2015

Creative Commons: Attribution 4.0


Source www.africanstorybook.org

Kuku na Jongoo

Brigid Simiyu
Magriet Brink



Kiswahili



Kuku na Jongoo
walikuwa marafiki.



Walienda kucheza
mpira wa miguu.




Kuku alikuwa
golikipa.



Jongoo alilifunga
bao.



Kuku alikasirika
sana.



Kuku aliamua
kummeza Jongoo.



Kuku alipoondoka
uwanjani,
alikutana na
Mama ya Jongoo.



Jongoo aliyemezwa
alilia, "Mama
nisaidie.
Nimemezwa."



Jongoo alikuwa na
ladha mbaya sana.
Kuku alihisi
kichefuchefu.



Kuku alikohoa na
kumtema Jongoo.



Jongoo
alipotemwa,
alitoroka na
kwenda zake.



Kuku na Jongoo
walikuwa maadui
tangu siku hiyo.

Kuku na Jongoo

Author - Winny Asara

Translation - Brigid Simiyu

Illustration - Magriet Brink

Language - Kiswahili

Level - First words

© African Storybook Initiative 2014

Creative Commons: Attribution 4.0

Source www.africanstorybook.org


ASb
approved

Kusema Asante!


Ursula Nafula
Rob Owen



Kiswahili




Mtu, Simba, Mbwa,
Nyoka, Tai na
Punda walienda
vita.



Yona na mkewe
waliwakaribisha
kwao.

Wakawachinjia
ng'ombe wao.




Kila mmoja alitaka
sehemu tofauti ya
ng'ombe.

Waliahidi kuwapa
zawadi.



Yona na mkewe
walimpa kila
mmoja sehemu ya
nyama aliyotaka.



Baada ya kula,
walilala vizuri.

Asubuhi, walienda
zao.



Wiki nyingi zilipita.

Simba akawaletewa
zawadi ya pembe
kubwa ya tembo.



Mbwa akasema,
"Zawaidi yangu
itakuwa
kuwachungia
pembe hii ili
isiibwe."



Ndugu wa Yona
akawaza, "Nitaiba
ile pembe niiuze."



Alipoenda kuiba ili pembe, Nyoka alimuuma.



Yona na mkewe
wakachukua
mifugo wa
mrehemu.

Wakawa matajiri.



Tai akawaona
wafanya biashara.

Walibeba pesa na
vito vya bei.



Tai akazinyakua
zile pesa na vito.

Akawapelekea
Yona na mkewe.



Punda alichoka
kumbebea tajiri
wake gunia nzito la
pesa.



Akawapelekea
Yona na mkewe lile
gunia la pesa.

"Nashukuru
mlivyonisaidia."



Yona akasema,
"Wanyama
wametupa zawadi
zao. Lakini, Mtu
hajafanya hivyo."



Walingonja,
wakangoja, lakini,
Mtu hakuwaletea
zawadi yake
alivyoahidi.

Kusema Asante!

Author - Mariam Mohammed and Elizabeth Laird

Translation - Ursula Nafula

Illustration - Rob Owen

Language - Kiswahili

Level - First words

© African Storybook Initiative 2016

Creative Commons: Attribution 4.0

Source www.africanstorybook.org

Original source www.ethiopianfolktales.com

Kutotii!


Brigid Simiyu
Marion Drew





Ulikuwa wakati wa wanyama kwenda kulala.

Mmoja wao hakutii.



Mkulima
alimwambia Piggy
aende kulala.

Piggy alikataa.



Mkulima
alimwuliza Trasti
Wip kumcharaza
Piggy.

Trasti Wip alikataa.



Moto Kali alikataa
kumtekeza Trasti
Wip kwa kutotii.



Maji Safi hakumtii
mkulima.

Alikataa kumzima
Moto Kali.



Mkulima
alimwuliza
Ng'ombe Moo
kunywa Maji Safi.



Ng'ombe Moo
alisema,
"Nitayanywa maji
haya. Nina kiu."



Maji Safi alilia,
"Usininywe.
Nitamzima Moto
Kali."



Moto Kali alipiga
kelele, "La,
hutanizima.
Nitamteketeza
Trasti Wip."



Trasti Wip alilia,
"Tafadhali
usiniteketeze.
Nitamcharaza
Piggy."



Piggy alisema kwa
hasira,
"Usinicharaze.
Nitaingia
chumbani."



Piggy aliingia
chumbani tayari
kulala.

Kutotii!

Author - Thobile Gama

Translation - Brigid Simiyu

Illustration - Marion Drew

Language - Kiswahili

Level - First words

© African Storybook Initiative 2016

Creative Commons: Attribution 4.0

Source www.africanstorybook.org



ASb
approved

Kuwahesabu Wanyama

Susan Kavaya
Rob Owen


Kiswahili



Tembo mmoja
anaenda kunywa
maji.



Twiga wawili
wanakaribia
kunywa maji.




Nyati watatu na
ndege wanne pia
wandaenda kunywa
maji.



Swala watano na
nguruwe mwitu
sita wanafika
mahali kuna maji.



Pundamilia saba
wanakimbia
kwenda kunywa
maji.



Chura wanane na
samaki tisa
wanaogelea
majini.



Simba mmoja
ananguruma.
Anataka kunywa
maji.

Ni nani
anamwogopa
simba?



Tembo mmoja na
simba mmoja
wanakunywa maji
pamoja.

Kuwaheسابu Wanyama

Author - Zanele Buthelezi, Thembani Dladla and Clare Verbeek

Translation - Susan Kavaya

Illustration - Rob Owen

Language - Kiswahili

Level - First words

© School of Education and Development (Ukzn) and African Storybook Initiative 2007

Creative Commons: Attribution 4.0

Source www.africanstorybook.org

Original source www.akdn.org

Magezi na Kasiira

Brigid Simiyu
Brian Wambi



Kiswahili



Magezi na Kasiira
waliishi pamoja.

Walishiriki chakula
pamoja.



Magezi alisema,
"Tulime pamoja
jinsi tunavyokula
pamoja."



Magezi
alimwambia
Kasiira, "Wewe
lima mimi
nitapanda."



Magezi pia
alimwambia
Kasiira, "Wewe
panda mimi
nitapalilia."



Mtama ulikomaa.

Kasiira
alimwambia
Magezi avune.



Magezi alijibu,
"Wewe vuna. Mimi
nitahifadhi."



Magezi alikuwa
mvivu.

Kasiira alimpatia
kifungu kimoja tu
cha mtama.



Magezi alikutana
na Kuku.



Kuku alikula ule
mtama.

Alimpatia Magezi
yai.



Magezi aliwakuta
watoto wekicheza.

Walilivunja lile yai.



Watoto walimpatia
Magezi embe.



Magezi alimkuta
Kasuku.

Kasuku alilikula
embe kisha
akampatia unyoya.



Ziwa liliuchukua
unyoya.

Likampatia Magezi
maji.



Magezi aliyatumia
maji kuzima moto
wa wachoma
makaa.



Wachoma makaa
walimpatia Magezi
shoka.



Magezi aliwakuta
wachinjaji.

Waliivunja shoka.



Magezi alipatiwa
kichwa na mkia wa
fahali.

Ona alichofanya
Magezi!



Alipiga mayowe,
"Fahali wa mfalme
amekwama
matopeni!"

Ulikuwa ujanja tu.



Watu walikuja
kumsaidia.

Magezi
aliwaambia,
"Vuteni mkia na
kichwa."



Magezi aliwaambia watu, "Nipeni ng'ombe wenu nimpelekee mfalme."

Magezi na Kasiira

Author - Cornelius Gulere

Translation - Brigid Simiyu

Illustration - Brian Wambi

Language - Kiswahili

Level - First words

© Text: Uganda Community Libraries Association (Ugcla) Artwork: African Storybook Initiative 2015

Creative Commons: Attribution 4.0

Source www.africanstorybook.org

Original source <http://ugcla.org>

ASb
approved




Mamba aliyekuwa na njaa

Brigid Simiyu
Wiehan de Jager



Wakati mmoja
palikuwa na
mamba aliyekuwa
na njaa.



Alikitafuta chakula
polepole tena
kimya kimya.

Halafu.




PUU! Mamba
alishambulia!



Baadaye, hakuwa
na njaa tena.

Alifurahi.



Alitulia hadi
alipohisi njaa tena.

Mamba aliyekuwa na njaa

Author - Christian G.

Translation - Brigid Simiyu

Illustration - Wiehan de Jager

Language - Kiswahili

Level - First words

© Christian G. 2014

Creative Commons: Attribution 4.0

Source www.africanstorybook.org

Mamba na Mbwa

Brigid Simiyu
Rob Owen



Kiswahili



Siku moja, Mbwa aliyapata mayai kando ya mto.




Mbwa aliyaweka
mayai hayo kumi
katika kikapu.



Mbwa aliyalinda na
kuyaweka mahali
kwenye joto.



Mamba alimwuliza
Mbwa, "Umeyaona
mayai yangu?"



Mamba aliwauliza
wanyama wote
ikiwa waliyaona
mayai yake.



Wakati huo, mayai
yaliangua moja
moja.



Mbwa hakuweza
kuwapa mamba
wachanga chakula
cha kutosha.



Siku moja, Mamba
aliyasikia
matumbo ya
wanawe
yakinguruma!



Mamba aliingia
nyumbani
akamcharaza
Mbwa kwa mkia
wake.



Mamba
alimkimbiza Mbwa
barabarani.



Mbwa alisimama
akamwambia
Mamba,
“Nisamehe!”



Mamba
alimsamehe.
Alienda na wanawe
kuogelea.

Mamba na Mbwa

Author - Candiru Enzikuru Mary

Translation - Brigid Simiyu

Illustration - Rob Owen


Language - Kiswahili

Level - First words

© African Storybook Initiative 2016

Creative Commons: Attribution 4.0

Source www.africanstorybook.org



Mbweha asiye na shukurani


Brigid Simiyu
Jacob Kono

Kiswahili



Mbweha alikuwa
na njaa.

Alienda kuwinda.




Alimfukuza panya.

Panya alijificha
chini ya jiwe.



Mbweha alichimba
kumtoa panya.

Jiwe liliangukia
mguu wake.




Sungura alimsikia
Mbweha akilia.

Alikimbia kuona
kilichotokea.



Sungura alikubali
kumsaidia
Mbweha.

Mbweha aliahidi
kumpatia chakula.



Sungura
alilisukuma jiwe.

Liliondoka kwenye
mguu wa Mbweha.




Sungura alim dai
zawadi yake.


Mbweha alitisha
kumla Sungura!



Walimtafuta mzee
kuwaamulia kesi
yao.



Mbweha alitisha
kumla yule mzee
pia!



Mzee alisema,
"Hebu nione lile
jiwe kabla
kuamua."



Mbweha na
Sungura
walimwonyesha
mzee lile jiwe.



Mbweha alieleza
jinsi jiwe liliangukia
mguu wake.



Mzee alimwuliza
Sungura,
"Nionyeshe namna
ulivyolisukuma
jiwe."



Sungura
alilisukuma jiwe.

Liliangukia mguu
wa Mbweha.



Mzee alisema,
"Sasa ni sawa.
Hebu twende
nyumbani."



Mzee na Sungura
walienda zao.

Mbweha aliachwa
akiwa amenaswa.

Mbweha asiye na shukurani

Author - Mohammed Kuyu and Elizabeth Laird

Translation - Brigid Simiyu

Illustration - Jacob Kono

Language - Kiswahili

Level - First words

© African Storybook Initiative 2016

Creative Commons: Attribution 4.0


Source www.africanstorybook.org

Original source www.ethiopianfolktales.com

ASb
approved

Meno aina
gani?
Brigid Simiyu


Kiswahili



Mamba ana meno
makali.



Simba pia ana
meno makali.



Papa ana meno
makali sana.

Kwa nini baadhi ya
wanyama wana
meno makali?



Ng'ombe ana
meno yenye nguvu.

Anayatumia
kusaga chakula.



Ndege hawana
meno.


Wao hula namna
gani?



Panya wana meno
makubwa ya
mbele.



Kitambo, nilikuwa
na meno ya mbele.



Meno yangu ya
mbele yaling'oka!

Je, wewe una meno
mangapi?

Meno aina gani?

Author - Zanele Buthelezi, Thembani Dladla and Clare Verbeek

Translation - Brigid Simiyu

Illustration - and Rob Owen

Language - Kiswahili

Level - First words

© School of Education and Development (Ukzn) and African Storybook Initiative 2007

Creative Commons: Attribution 4.0

Source www.africanstorybook.org

Original source www.akdn.org

Mfalme mbaya

Ursula Nafula
Marleen Visser



Kiswahili



Mbuzi alikuwa
mfalme wa
wanyama na
ndege.

Aliita mkutano.




Mbuzi aliwaambia
kwamba aliota
ndoto.

Wote walisikiliza.



Ndoto ilihusu njaa.

"Tutafanyaje?"
Paka aliuliza.



Kuku na Bata
walisema, "Ni
vyema sisi kuweka
chakula kwa
mfalme."




Mfalme Mbuzi
alisema, "Mfunge
yeyote
atakayekataa
kutii."



Wakati wa
kumchagua
mfalme mpya
ulifika.

Walimchagua
Paka.



Mbuzi hakutaka
Paka kuwa
mfalme.

"Mimi ndiye
mfalme."



Mbuzi alikataa
kupeleka chakula.

Ng'ombe aliuliza,
"Tutafanyaje?"



Wanyama na
ndege walijadili
pamoja.

Walimkasirikia
Mbuzi.



Mbwa alisema,
"Nilikuwa naye
wakati wote
alipokuwa
mfalme."



Kondoo akasema,
"Niliwapatia
watoto wake sufu
yangu nyororo."



Nguruwe alilila,
"Alipokuwa
mfalme,
nilimchungia
bustani yake."



"Kwani Mbuzi
alifikiri atakuwa
mfalme milele?"
Kondoo aliuliza.



Wanyama
walikubaliana.

Lazima Mbuzi
apeleke chakula
kwa mfalme Paka.



Walipomkuta
Mbuzi, aliwaambia,
"Nitakuwa mfalme
wakati wote."



Wanyama
walimjibu,
"Tutakufunga
tukupeleke kwa
mfalme mpya."



Ng'ombe alimvuta
Mbuzi kumpeleka
kwa mfalme.

Wengine
walishangilia.

Hiyo ndiyo sababu
mbuzi hukataa
kusonga
wanapovutwa.



Mfalme mbaya

Author - Alice Nakasango

Translation - Ursula Nafula

Illustration - Marleen Visser

Language - Kiswahili

Level - First words

© Text: Uganda Community Libraries Association (Ugcla) Artwork: African Storybook Initiative 2015

Creative Commons: Attribution 4.0

Source www.africanstorybook.org

Original source <http://ugcla.org>



Mtoto na Korongo

Brigid Simiyu
Emily Berg



Mama na baba
walienda
shambani.

Walimwacha
Makabi amchunge
mtoto.



Makabi alicheza
akasahau
kumlinda mtoto.

Korongo walimkuta
mtoto akilia.




Walimbebea ndani
ya blanketi
wakaruka naye
juu.





Mama aliwaona
korongo wanne
wakiruka.

Walikuwa
wamembeba
mtoto wake.



Korongo
walimlinda mtoto
vyema.

Korongo
walipotoka, chura
alimmeza mtoto!





Chura alitaka
zawadi ili
amrudishe mtoto.

Alipewa nzi watatu.

Mtoto na Korongo

Author - South African Folktale

Translation - Brigid Simiyu

Illustration - Emily Berg

Language - Kiswahili

Level - First words

© African Storybook Initiative 2014

Creative Commons: Attribution 4.0

Source www.africanstorybook.org

Mvulana asiyetii


James Elim
Wiehan de Jager



Kiswahili



Kijiji kimoja
kilikuwa karibu na
msitu.



Msitu huo ulikuwa
na fisi na wanyama
wengine wakali.



Watu wengi
walivamiwa na fisi.



Ekeno alionywa na
wazazi asiende
mbali na
nyumbani.




Ekeno alipuuza
ushauri wa wazazi.
Siku moja alienda
kutafuta asali.



Alitembea kwa
muda mrefu.
Alijipata akiwa
mahali asikokujua.



Usiku, alitafuta
mahali pa kulala.



Usiku wa manane,
Ekeno aliamua
kuitafuta njia ya
kurudi nyumbani.



Alivamiwa na fisi
wakamla.



Wenzake walienda
kumtafuta.



Jirani mmoja
aliwaelekeza kuwa
Ekeno aliingia
msituni.



Waliamini kuwa
alikuwa ameliwa
na fisi.

Mvulana asiyetii

Author - James Elim and Joseph Opilo

Illustration - Wiehan de Jager, Benjamin Mitchley, Catherine Groenewald and Padmanabha

Language - Kiswahili

Level - First words

© African Storybook Project 2014

Creative Commons: Attribution 4.0

Source www.africanstorybook.org



Mwanamume na mwanamke wa kwanza


Mutugi Kamundi
Jemma Kahn

Kiswahili




Zamani dunia
ilikuwa mpya.

Milima ilifunika
ulimwengu kama
blanketi.




Dunia ilikuwa na
dimbwi kubwa.

Lilikuwa na maji
baridi yaliyotulia.




Nyoka wawili
waliishi kwenye
dimbwi.

Mmoja mwenye
nguvu, mwingine
dhaifu.



Siku moja radi
ilipiga.

Nyoka wakaona
ardhi na vitu
tofauti.



Wakaamua
kwenda kuishi
kwenye ardhi.




Wakajikunjua
wakaogelea.

Wakaelekea
kwenye
mwangaza.



Mikia yao
ikagawika wakawa
na miguu.

Wakapata pia
mikono na vidole.



Wakageuka
wakawa mume na
mke.

Wakatazamana,
wakapendana.



Wakaamua kulinda
wanyama na
mimea.

Wakafurahia jua.



Wakashikana
mikono.

Wakatembea
pamoja kwenye
ulimwengu wao
mpya.

Mwanamume na mwanamke wa kwanza

Author - Southern African Folktale

Translation - Mutugi Kamundi

Illustration - Jemma Kahn

Language - Kiswahili

Level - First words

© African Storybook Initiative 2014

Creative Commons: Attribution 4.0

Source www.africanstorybook.org



Ng'ombe wetu Pendo

Ruth Odondi
Rob Owen




Jina langu ni Ndalo.



Baba yangu
anamfuga
ng'ombe.

Anaitwa Pendo.



Pendo hupenda
kula nyasi siku
nzima.



Wakati mwingine
baba humpa
Pendo nafaka.



Pendo pia hunywa
maji mengi.



Mimi ninampenda
Pendo.



Baba humkama
Pendo.

Sisi humtunza
Pendo naye
hutusaidia.



Pendo hutupa
maziwa mengi.



Mimi hunywa
maziwa mengi.



Baba huuza
maziwa.

Hutumia pesa hizo
kuninunulia vitabu
vya hadithi.



Mimi hupenda
kusoma hadithi.



Umefahamu kwa
nini ninampenda
ng'ombe wetu
Pendo?

Ng'ombe wetu Pendo

Author - Ruth Odondi

Illustration - Rob Owen

Language - Kiswahili

Level - First words


© African Storybook Initiative and Molteno Institute, 2014

Creative Commons: Attribution 4.0

Source www.africanstorybook.org




Ni nani
atakuwa
mfalme?
Ursula Nafula
Salim Kasamba



Mfalme Chui
aliendelea kuwa
mzee.

Je, atamchagua
mrithi wake namna
gani?




Mfalme Chui
aliwaita wanyama
kwa sherehe.

Atawatangazia
mpango wake.




Baada ya sherehe,
Mfalme Chui
alizungumza.

Wanyama
walimsikiliza.



Alisema,
"Mashindano
yataamua
atakayekuwa
mfalme."



Atakayehesabu
hadi kumi kabla ya
mkuki kuanguka,
atakuwa mfalme.



Tembo
aliwasukuma
wengine, "Mimi ni
mkubwa.
Ninastahili kuwa
mfalme."




Tembo alihesabu
hadi nne pekee.

Mkuki ulianguka.



Ngiri aliwasukuma
wenzake akisema,
"Nina nguvu zaidi.
Nitakuwa mfalme."



Ngiri alihesabu
hadi sita kisha
mkuki ulianguka.

Aliondoka.



Wanyama
walisema, "Tembo
mkubwa na Ngiri
wameshindwa.
Nani atashinda?"



Sokwe alihesabu,
"Moja! Mbili! Tatu!
Nne! Tano! Sita!
Saba!"

Alilia.



Mfalme Chui
alisema, "Sokwe,
unapate nafasi
moja tu."

Sokwe aliondoka.




Baadhi ya
wanyama walianza
kuondoka.

Swara Mdogo
alisema, "Hebu
njaribu."



Mfalme Chui
aliwakemea,
"Mpeni Swara
nafasi. Mwache
ajaribu."



Swara alisema,
"Tano na tano ni
kumi."

Mkuki ulianguka
chini.



Mashindano
yalionyesha
mnyama mwerevu.

Swara alikuwa
malkia baada ya
chui.

Ni nani atakuwa mfalme?

Author - Athieno Gertrude and Owino Ogot

Translation - Ursula Nafula

Illustration - Salim Kasamba

Language - Kiswahili

Level - First words

© African Storybook Initiative 2017


Creative Commons: Attribution 4.0

Source www.africanstorybook.org




Nyani
aliyekuwa chifu
Ursula Nafula
Isaac Okwir

Kiswahili




Don alikuwa nyani
mkubwa.


Alikuwa mchokozi.




Don ndiye alikuwa
chifu wa nyani
wengine.




Wafuasi wake
walimpatia
kitambaa maalum.



"Nitakivaa
kichwani," Don
alisema.



"Kila mmoja afuate
masharti yangu.
Msinihoji!"
Don alipiga kelele.




Wafuasi
walimfuata chifu
wao.

Don iliporuka, kila
mmoja aliruka.




Lakini, kile
kitambaa,
kilimkaza sana.




Don aligusa kichwa
alikoumia.

Nyani pia waligusa
vichwa vyao.




"Hapa panuma,"
Don alisema.

Nyani pia
walisema, "Hapa
panauma."




Alisema, "Hii
imekazika sana!"

Wao pia walisema,
"Hii imekazika
sana."



Don alianguka
kutoka juu.

Wote walimuiga
wakaanguka.



Nyani aliyekuwa
chifu alikufa.

Wafuasi wake
waliumia, lakini
waliishi.

Nyani aliyekuwa chifu

Author - Bonsamo Miesso and Elizabeth Laird

Translation - Ursula Nafula

Illustration - Isaac Okwir

Language - Kiswahili

Level - First words

© African Storybook Initiative 2016

Creative Commons: Attribution 4.0

Source www.africanstorybook.org

Original source www.ethiopianfolktales.com

Nyumbu

Brigid Simiyu
Marleen Visser



Kiswahili



Hapo zamani,
kulikuwa na
nyumbu mrembo.

Aliitwa Waridi.



Farasi mwenye
umbo zuri alisema,
"Lazima nimwoe
Waridi."



Farasi alimwambia
Waridi, "Twende
mtoni pamoja."



Farasi alimwuliza
Waridi kuwa mke
wake.

Waridi alikubali.



Farasi alitaka
kumfahamu Waridi
zaidi.

Alimwuliza,
"Wazazi wako ni
nani?"



Waridi alijibu,
"Mama yangu
anaishi katika ikulu
ya mfalme."



"Dada yangu
anaishi katika
uwanja wa kanisa.
Kwani humjui?"



Aliongeza,
"Shangazi yangu
mrembo anaishi na
mzee wa kijiji."



Wakati huo, punda
mzee alipita.
Alikuwa babake
Waridi.



Waridi
hakumsalimu
babake wala
hakumtazama.



Punda yule mzee
akauliza, "Kuna
nini binti yangu?"



Farasi alimwuliza
Waridi, "Huyu
punda mjinga ni
nani?"



Waridi alimjibu,
"Mimi simjui."



Farasi alimpiga
teke yule punda
mzee.



Punda mzee
alivunjika moyo.

Alilia kisha akafa.



Waridi
hakumheshimu
babake.

Hii ndiyo sababu
nyumbu hawazai
watoto.

Nyumbu

Author - Mesfin Habte-Mariam and Elizabeth Laird

Translation - Brigid Simiyu

Illustration - Marleen Visser

Language - Kiswahili

Level - First words

© African Storybook Initiative 2016

Creative Commons: Attribution 4.0

Source www.africanstorybook.org

Original source www.ethiopianfolktales.com

Panya na Paka

Brigid Simiyu
Jacob Kono



Kiswahili



Hapo zamani, paka
na panya walikuwa
marafiki.



Panya walianza
kupoteza baadhi
ya jamaa zao.



Panya mmoja
mzee alisema,
"Nadhani paka
wanatula."



Akina mama
waliwaambia
watoto wao, "Kueni
waangalifu.
Msiende nje."



Panya wote
walikuwa
waangalifu.

Waliketi ndani ya
mashimo yao.



Paka walianza
kuwa na njaa.

Waliuliza, "Panya
wako wapi?"



Paka
waliwatembelea
panya.


Walitaka kupanga
harusi kati yao.



Walisema,
"Tungependa binti
wenu mmoja
aolewe kwa
mvulana wetu."



Panya
waliwaambia paka,
"Mnadanganya.
Mnataka kutula."




Mwishowe,
walikubali kuwa na
harusi kati ya
wanao.




Paka walirudi
nyumbani kwa
furaha.

Walilamba midomo
yao.



Siku ya harusi,
panya walikuwa
waangalifu sana.



Paka waliwasili
wakiimba wimbo
wa harusi.



Wimbo ulisema,
"Washikeni
muwale."



Panya mzee
alianza kuimba,
"Kimbieni, panya,
kimbieni."



Panya mzee
aliwaambia paka,
"Sisi nanyi si
marafiki."

Panya na Paka

Author - Merga Debelo and Elizabeth Laird

Translation - Brigid Simiyu

Illustration - Jacob Kono

Language - Kiswahili

Level - First words

© African Storybook Initiative 2016

Creative Commons: Attribution 4.0

Source www.africanstorybook.org

Original source www.ethiopianfolktales.com

ASb
approved

Petros ampata rafiki

Ursula Nafula
Brian Wambi

Kiswahili



Petros alikuwa
mtoto wa pekee.

Alikuwa
mwanafunzi
mwerevu.



Siku moja, Petros alipata ruhusa ya kwenda kucheza na marafiki zake.



Alimuona mbwa
akiwa amekwama
shimoni.

Petros alisema,
"Nitakusaidia."



Mbwa alibweka,
akacheza na
kumlamba Petros
kwa furaha.



Marafiki za Petros
walimfukuza mbwa
huyo.

Petros alisema,
"Acha! Acha!"



Mbwa aliwaogopa
wale wavulana
akajificha.




Marafiki za Petros
walimkuta akilia.

Walimwambia,
"Tutamtafuta
mbwa wako."



Petros hakuwa na matumaini.

"Tutampata."
Marafiki zake
wakasema.



Walimtafuta kila mahali.

Petros alisema,
"Anaweza kuwa karibu na mto."



Mbwa alipowaona,
alitaka kuruka
mtoni.

Petros alimsihi,
"Usiruke majini!"



Mbwa alimkimbilia
Petros.

Walifurahi pamoja.



Marafiki za Petros
walimwambia,
"Tusamehe.
Atakuwa rafiki yetu
pia."

Petros ampata rafiki

Author - Bethelihem Waltenegus

Translation - Ursula Nafula

Illustration - Brian Wambi

Language - Kiswahili

Level - First words


© African Storybook Initiative 2017

Creative Commons: Attribution 4.0

Source www.africanstorybook.org

Punda na Fahali


Ursula Nafula
Salim Kasamba



Kiswahili



Mukulima alikuwa
na Fahali mzee.




Pia, alikuwa na
Punda.

Fahali na Punda
walikuwa marafiki.




Mwisho wa siku,
Fahali alimwambia
Punda, "Leo
nimechoka sana."




Siku iliyofuata,
Fahali tena
alilalamika, "Leo
sikupumzika hata
kidogo."



Punda alimjibu,
"Nilienda sokoni.
Kazi yangu ilikuwa
ngumu kuliko
yako."



Kesho yake Fahali alisema tena, "Leo ilikuwa siku mbaya kwangu."



Punda alimjibu,
"Mkulima akija,
mlilie, 'Moo! Moo!'
Atakuruhusu
upumzike."




Fahali alimlilia
mkulima, "Moo!
Moo!"

Mkulima
alimruhusu
akapumzika.




Mkulima alimfunga
Punda jembe.

Punda alilima
badala ya Fahali.




Punda alifanya kazi
siku nzima.

Jioni, alikuwa
amechoka sana.



Punda alisema,
"Mkulima
ameamua
kukuchinja.
Unachoka sana
tena u mgonjwa."



Fahali alimjibu
Punda, "Kesho
nitafanya kazi
yangu. Nimepata
nafuu."

Punda na Fahali

Author - Melese Getahun Wolde and Elizabeth Laird

Translation - Ursula Nafula

Illustration - Salim Kasamba

Language - Kiswahili

Level - First words

© African Storybook Initiative 2016

Creative Commons: Attribution 4.0

Source www.africanstorybook.org

Original source www.ethiopianfolktales.com



Siafu na Njiwa
mvivu
Ursula Nafula
Joe Werna



Siafu alikuwa
mkulima mzuri.

Aliishi kwenye
ardhi na familia
yake.



Walifanya bidii
katika shamba lao.

Familia ya Siafu
iliishi vizuri.



Njiwa alikuwa jirani
ya Siafu.

Njiwa aliishi
kwenye mti na
familia yake.



Njiwa na familia
yake hawakulima.

Walistarehe
mchana kutwa.



Njiwa na familia
yake waliimba
vizuri.




"Mtatugawia
chakula?" Njiwa
aliuliza.

"La! Limeni chenu!"
Siafu alijibu.



Njiwa aliruka chini
na kuanza kuimba,
"Siafu ni mfalme!"



"Siafu ni mfalme!
Siafu ni mfalme!
Siafu ni mfalme!"

Siafu alifurahi.



Walipewa chakula.

Baada ya kula,
Njiwa na familia
yake walirudi
kwao.



Kesho yake, Njiwa
alimkejeli Siafu.

"Kwani wafalme
wana vichwa
vikubwa?"



"Huna shukuruni.
Tena wewe ni
mvivu!" Siafu
alilalamika.



"Samahani!" Njiwa
alisema, halafu
akaanza kuimba,
"Siafu ni mfalme!"

Siafu na Njiwa mvivu

Author - Terkule Aorabee

Translation - Ursula Nafula

Illustration - Joe Werna


Language - Kiswahili

Level - First words

© African Storybook Initiative 2018

Creative Commons: Attribution 4.0

Source www.africanstorybook.org



Simba Jike na Mbuni

Brigid Simiyu
Brian Wambi

Kiswahili



Mbuni na Simba
Jike walikuwa
marafiki wakati
mmoja.



Mbuni aliwalisha
wanawe vyema.

Walikuwa wenye
afya nzuri.



Watoto wa Simba
Jike walikonda.

Hawakupata
chakula cha
kutosha.



Simba Jike
alitamani
vifaranga wa
Mbuni kuwa wake.



Siku moja, Mbuni alikwenda safari.

Simba Jike alichukuwa vifaranga wake.



Mbuni aliporudi,
aliuliza, "Watoto
wangu wako
wapi?"



Mbuni alimkuta
Simba Jike na
watoto wake.




Simba Jike
alimwambia,
"Vifaranga ni
wangu sasa.
Wachukue wana
simba."




Mbuni alijiuliza,
"Nitawapataje
wanangu?"



Mbuni aliitisha
mkutana wa
wanyama wote.



Wanyama walifika
kuhudhuria
mkutano.



Tembo aliwauliza
Mbuni na Simba
Jike kujieleza.



Wanyama wengi
waliogopa
kumulaumu Simba
Jike.



Kichakuro alisema,
"Watoto
wanaofanana na
ndege, ni wa
Mbuni."



Baada ya kusema hivyo, Kichakuro alitoroka akaingia shimoni.



Simba Jike
alikasirika sana.

Alirudi kwake na
wana simba.

Simba Jike na Mbuni

Author - Daniel Nanok

Translation - Brigid Simiyu

Illustration - Brian Wambi

Language - Kiswahili

Level - First words

© African Storybook Initiative 2016

Creative Commons: Attribution 4.0


Source www.africanstorybook.org

Sokwe na Mamba


Brigid Simiyu



Kiswahili




Sokwe alimkuta
Mamba kando ya
ziwa.



Akamwuliza
Mamba, "Unaishi
wapi?"

Mamba akamjibu,
"Ziwani."



Mamba
akamwuliza,
"Wewe unaishi
wapi?"

Sokwe akamjibu,
"Kwenye miti."



Mamba akataka
kumjua Sokwe
zaidi.

Akamwuliza,
"Unaweza
kuogelea?"



"Siwezi," Sokwe
akamjibu.

Mamba akasema,
"Nitakufunza."



Mamba akasema,
"Sisi sasa ni
marafiki.
Usiogope."




Mamba akasema,
"Mjomba ni
mgonjwa. Anahitaji
nyama ili apone."



Sokwe akaogopa
sana.


Je, Mamba
atamula?



Sokwe akataka
kumtoroka
Mamba.




Sokwe akapata
wazo zuri.



"Nitautoa moyo
wangu umpatie,"
Sokwe akaahidi.



"Lakini moyo
wangu uko mtini,"
Sokwe akasema.



"Utauleta moyo wako?" Mamba akauliza.

Sokwe akamjibu, "Ndiyo."




Mamba akaogelea
kutoka majini.

Sokwe akakimbilia
kwenye miti.



"Wewe si rafiki
yangu.
Ulinidanganya!"
Mamba akasema.



"Hatuko marafiki.
Unataka kunila!"
Sokwe akamjibu.

Sokwe na Mamba

Author - Mulualem Daba

Translation - Brigid Simiyu

Illustration -

Language - Kiswahili

Level - First words

© African Storybook Initiative 2016


Creative Commons: Attribution 4.0

Source www.africanstorybook.org




Sungura amdanganya Tembo


Ursula Nafula
Wiehan de Jager




Tembo na Sungura
walikuwa marafiki.



Walilisha mifugo
yao sehemu
iliyokuwa na nyasi
na maji.



Walizoea kucheza
mpira wa miguu.



Tembo alifunga
mabao mengi.

Sungura
hakufurahi.




Sungura aliuliza,
"Nini inakusaidia
kucheza vyema?"

"Miguu yangu
minono."




Sungura na Tembo
walishindana mbio.

Sungura alishinda.



Alimwuliza, "Nini
inakusaidia
kwenda mbio?"

"Miguu yangu
myembamba."



Tembo alimwuliza
Sungura,
"Nitapataje miguu
myembamba?"

"Nitakuonyesha."




Sungura alisema,
"Simama ndani ya
moto."


Tembo alilia,
"Ninaungua!"




Sungura alisema,
"Hii ndiyo njia
pekee ya kuipata
miguu
myembamba."




Tembo alilala chini.



Kwa siku nyingi,
hakuweza
kusimama.



Alipopata nafuu,
alienda nyumbani
kwa familia yake.



Sungura alisikitika
sana.

Alimwomba Tembo
msamaha.

Sungura amdanganya Tembo

Author - Agnes Gichaba

Translation - Ursula Nafula

Illustration - Wiehan de Jager

Language - Kiswahili

Level - First words

© African Storybook Initiative 2015

Creative Commons: Attribution 4.0

Source www.africanstorybook.org

Sungura na Fisi

Brigid Simiyu
Rob Owen




Kiswahili



Sungura na Fisi
walikuwa marafiki.

Walifanya kazi na
kucheza pamoja.



Sungura alisema,
"Tulime pamoja."

Fisi akamwuliza,
"Tutapanda nini?"



Sungura
aliwachunga
ndege wasile
mahindi.

Fisi alikuwa alime
shamba.




Fisi alilalamika.

Sungura akamjibu,
"Nitawafukuza
ndege wakati
wote."



Fisi alikubali
kulilima shamba.

Alipomaliza,
alipanda mbegu ya
mahindi.



Fisi alipalalia
mahindi.

Sungura aliketi juu
ya jiwe akiimba.



Sungura
aliwafukuza ndege
kwa furaha.

Hakutoa jasho
hata kidogo.



Sungura alisema,
"Nitavuna kilicho
juu ya udongo.
Nawe kilicho chini."



Sungura
alitangulia
kuyavuna mahindi.

Fisi alikuwa wa
mwisho.



Fisi alipata mizizi
pekee.

Aliwaza kwa muda
mrefu.



Fisi aligundua
kuwa Sungura
alimdanganya.

Alisema, "Tulime
tena pamoja."



Fisi alisema,
"Nitavuna
vinavyomea juu
nawe vinavyomea
chini ya udongo."



Wote walilima na
kupanda viazi.

Walifanya kazi zote
shambani pamoja.



Fisi alienda kuvuna
vilivyomea juu ya
ardhi.

Alipata majani
pekee.



Sungura alivuna
viazi vingi.

Fisi alikasirika,
"Kwa nini
ulinidanganya?"



Fisi alimfukuza
Sungura kulipiza
kisasi.

Tangu hapo,
wakawa maadui.

Sungura na Fisi

Author - Mutugi Kamundi

Translation - Brigid Simiyu

Illustration - Rob Owen

Language - Kiswahili

Level - First words

© African Storybook Initiative 2014

Creative Commons: Attribution 4.0

Source www.africanstorybook.org




Sungura na Fisi wanapanda mimea

Brigid Simiyu
Rob Owen



Hapo zamani,
Sungura na Fisi
walikuwa marafiki
wazuri.



Sungura
alimwambia Fisi,
“Ningependa
tulime pamoja.”




Sungura alionelea
wapande mahindi
na wagawane
majukumu.



Sungura
alimwambia Fisi,
"Kazi yangu ya
kuwafukuza ndege
ni ngumu."



Fisi alikubali kulima
shamba peke yake.



Wakati Fisi aling'oa
magugu, Sungura
aliketi chini
akiimba.



Mahinid
yalipokuwa tayari,
Sungura alifurahi
kuwafukuza ndege.



Sungura alisema,
“Nitavuna yaliyo
juu ya udongo.
Utavuna yaliyo
chini.”



Sungura alivuna
mahindi yote
akahifadhi.



Fisi alikuta mizizi
tupu chini ya
udongo.



Fisi aligundua
kwamba alikuwa
amedanganywa.

Alikasirika sana.



Walipanda viazi.
Fisi alisema,
“Nitavuna yaliyo
juu ya
udongo.”



Walifanya kazi
pamoja shambani
wakiimba.



Wakati wa kuvuna,
Fisi alivuna majani
ya viazi pekee.



Sungura alivuna
viazi vingi vikubwa
akahifadhi.



Fisi alimkimbiza
Sungura akitaka
kulipiza kisasi.

Urafiki wao uliisha.

Sungura na Fisi wanapanda mimea

Author - Mutugi Kamundi

Translation - Brigid Simiyu

Illustration - Rob Owen

Language - Kiswahili

Level - First words

© African Storybook Initiative 2014

Creative Commons: Attribution 4.0

Source www.africanstorybook.org



Tarik na rafiki yake

Ursula Nafula
Isaac Okwir



Tarik na familia
yake waliishi mbali
na mji mkuu.



Tarik alikuwa na
mbwa aliyeitwa
Buchi.

Walikuwa marafiki
wakubwa.



Siku moja, Tarik na rafiki yake Bedilu waliwapeleka mifugo malishoni.



Bedilu alipenda
wacheze, lakini
Tarik alitaka
kusoma.



Mwishowe, Bedilu
na Tarik waliamua
kucheza.



Walipokuwa
wakicheza, kondoo
walitoweka.

Waliwatafuta kila
mahali.



Mbwa mwitu aliua
kondoo wa Tarik.

Tarik aliogopa
kuadhibiwa na
baba yake.



Tarik aliamua
kulala juu ya mti.

Buchi alilala karibu
na mti huo.



Usiku, fisi walipiga
kelele Tarik
akaogopa.



Tarik alianguka
kutoka mtini.

Alisikia kelele
karibu naye.



Wakati huo, radi
ilimlika anga.

Tarik alimwona
Buchi akiwa
anamlinda!



Tarik na Buchi
waliketi juu ya mti
hadi asubuhi.

Tarik na rafiki yake

Author - Biniam Asfaw

Translation - Ursula Nafula

Illustration - Isaac Okwir

Language - Kiswahili

Level - First words

© African Storybook Initiative 2017

Creative Commons: Attribution 4.0

Source www.africanstorybook.org



Ujanja wa Sungura

Brigid Simiyu
Abraham Muzee

Kiswahili



Sungura alimkuta
Tembo. Tembo
alikuwa amekibeba
chungu cha asali.



Tembo alimbeba
Sungura
mgongoni.

Sungura aliilamba
asali ya Tembo.



Walimpata Nyati
mtoni akinywa
maji.



Sungura aliwauliza
Tembo na Nyati,
"Nani kati yenu
aliye na nguvu
zaidi?"




Sungura alisema
kwamba alijua
namna
atakavyojua
ukweli.



Kwanza, Sungura
alimfunga Tembo
kamba kiunoni.



Kisha akamfunga
Nyati kamba ile ile
kiunoni.



Sungura alijificha
kwenye mti
akasema, "Haya!
Vuteni!"



Nyati na Tembo
walivuta. Tembo
akamvuta Nyati.



Nyati akamvuta
Tembo.

Hakuna
aliyeshinda.



Sungura aliikata ile
kamba karibu na
Nyati.

Tembo alianguka
kwa kishindo!



Sungura
alimshangilia Nyati
akisema, "Ni wewe
mwenye nguvu
zaidi."

Ujanja wa Sungura

Author - Dan Kaasha

Translation - Brigid Simiyu

Illustration - Abraham Muzee


Language - Kiswahili

Level - First words

© African Storybook Initiative 2016

Creative Commons: Attribution 4.0


Source www.africanstorybook.org



Ulimwengu
wetu

Ursula Nafula
Herminder Ohri

Kiswahili




Mungu alitaka mtu
wa kuulinda
ulimwengu wake.



Simba alijitolea akasema, "Mimi ni mfalme. Ninaweza kufanya kazi hiyo."




Kwa sauti, Tembo akasema, "Mimi ni mkubwa. Ninafaa kufanya kazi hiyo."




Papa naye
akafikiri, "Meno
yangu ni makali.
Ninafaa kuulinda
ulimwengu."




Tai akachekeka na
kusema, "Ninaruka
na kuona kila kitu.
Ninafaa zaidi."



Mwishowe, Mungu
akasema,
"Nitawaumba watu
waulinde
ulimwengu
wangu."




Kwa hivyo, Mungu aliwaumba wanaume na wanawake wenye ngozi nyeusi.




Wengine pia
walikuwa maji ya
kunde.



Na baadhi yao
walikuwa na ngozi
ya manjano.



Nao wengine
wakawa na ngozi
ya waridi.



Papa
aliwachekelea
watu akisema,
"Wataogelea
namna gani?"

Mungu
alitabasamu na
kusema,
"Watajifunza."



Ulimwengu wetu

Author - Herminder Ohri

Translation - Ursula Nafula

Illustration - Herminder Ohri

Language - Kiswahili

Level - First words

© Pratham Books 2014

Creative Commons: Attribution 4.0

Source www.africanstorybook.org

Original source www.prathambooks.org



ASb
approved

The Adventures of SUPERCOW

Volume 1

Danielle Bruckert



Vituko vya
Ng'ombe
Shujaa
Mutugi Kamundi
Danielle Bruckert

Kiswahili



Huyu ni
ng'ombe mtulivu.



Mchana yeye ni
ng'ombe wa
kawaida.

Hupeperusha tiara.



Au kucheza mpira.





Usiku yeye
hubadilika na
kuwa Ng'ombe
Shujaa.

Yeye huokoa
maisha.



Na kupambana na
uhalifu.





Wewe pia
ukiyafumba macho
yako kabisa, kisha
uwe na hamu
kubwa.



Huenda ng'ombe
akakutembelea
pia!



Vituko vya Ng'ombe Shujaa

Author - Danielle Bruckert

Translation - Mutugi Kamundi

Illustration - Danielle Bruckert

Language - Kiswahili

Level - First words

© Danielle Bruckert 2010

Creative Commons: Attribution-Non Commercial 3.0

Source www.africanstorybook.org

Original source <http://freekidsbooks.org>




Wanyama wa kufugwa

Ursula Nafula
Sandy Campbell

Kiswahili


Ben anafuga
wanyama.





Huyu ni ng'ombe.

Anataka chakula.



Huyu ni mbuzi.

Anakunywa maji.



Huyu ni farasi.

Anakimbia.




Huyu ni nguruwe.

Amemaliza chakula
chake.



Huyu ni kuku.

Ana vifaranga
watatu.



Huyu ni mbwa.

Anabweka sana.



Ben amebeba
maziwa.

Mbwa wake
anataka maziwa.

Wanyama wa kufugwa

Author - Jenny Katz

Adaptation - Ursula Nafula

Illustration - Sandy Campbell

Language - Kiswahili

Level - First words


© African Reading Matters 2003

Creative Commons: Attribution-Non Commercial 3.0

Source www.africanstorybook.org

Original source www.read.org.za



ASb
approved

Wanyama
wapata miguu
Brigid Simiyu
Wiehan de Jager

Kiswahili



Hapo zamani,
wanyama
hawakuwa na
miguu.



Maguru alikuwa
amewapatia miguu
watu pekee.



Maguru aliamua
kumpatia kila
mnyama miguu.




Wanyama walitaka
miguu ili
watembea na
kukimbia.



Ilikuwa vigumu
kwao kutambaa.



Siku ilifika.
Wanyama tofauti
walitambaa
kwenda kwa
Maguru.



Maguru aliwapatia
wanyama na
ndege miguu.



Baadhi ya
wanyama
walicheza.
Wengine
walianguka chini.



Walisema,
“Hatutatambaa
tena.”



Jongoo alikuwa wa
mwisho kwenye
mstari.



Maguru alimpatia
miguu yote
iliyokuwa imabaki.



Jongoo alisema
kwa furaha,
“Nitatembea
haraka kuwaliko
wengine.”



Baadaye, Nyoka
alifika. Alimsihi
Maguru,
“Tafadhali, nipe
miguu.”



Nyoka alimwambia
Maguru, "Nililala
kupita kiasi."



Maguru hakupata
miguu yoyote ya
kumpatia Nyoka.



Tangu siku hiyo,
Nyoka anasubiri
kupata miguu.

Wanyama wapata miguu

Author - Mutugi Kamundi

Translation - Brigid Simiyu

Illustration - Wiehan de Jager

Language - Kiswahili

Level - First words

© African Storybook Initiative 2015

Creative Commons: Attribution 4.0

Source www.africanstorybook.org

Wapi paka wangu?

Ursula Nafula
Bronwen Heath



Kiswahili



Paka wangu yuko
wapi?



Hebu nitazame
mvunguni mwa
kitanda.



Labda yuko juu ya
kabati.



Hebu nitazame
nyuma ya kochi.



Je, anaweza kuwa
karibu na pipa la
takataka?



Je, anaweza kuwa
amejificha
kikapuni?



Hebu nimtafute nje
ya nyumba.



Aaa! Paka wangu
ndiye huyu hapa!

Wapi paka wangu?

Author - Clare Verbeek, Thembani Dladla and Zanele Buthelezi

Translation - Ursula Nafula

Illustration - Bronwen Heath

Language - Kiswahili

Level - First words

© School of Education and Development (Centre for Adult Education), University of Kwazulu-Natal 2007

Creative Commons: Attribution-Non Commercial 3.0

Source www.africanstorybook.org

Original source <http://cae.ukzn.ac.za/resources/seedbooks.aspx>






Watazame Wanyama

Caren Echesa
Sandy Campbell


Kiswahili

Tazama wanyama.





Ng'ombe anasema,
"Moo."



Mbuzi anasema,
"Meee, meee."



Farasi anasema,
"Nei."



Nguruwe
anasema,
"Ghuranti."



Kuku anasema, "Ko
ko. Ko ko."



Mbwa anasema,
"Bwa. Bwa."



Mkulima anasema,
"Kimya."

Watazame Wanyama

Author - Jenny Katz

Translation - Caren Echesa

Illustration - Sandy Campbell

Language - Kiswahili

Level - First words

© African Reading Matters 2003

Creative Commons: Attribution-Non Commercial 3.0

Source www.africanstorybook.org

Original source www.read.org.za

Kitabu hiki kimeandaliwa na:



Elimu Yetu

Soma zaidi:



maktaba.org